JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI MOUNT CHAFUKWE,
S.L.P 55
CHIMALA – MBEYA.
04/12/2020

KUMB NA. MTCSS/JI/2021
JINA LA MWANAFUNZI: _____

JINA LA SHULE ATOKAYO: _____

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA MOUNT CHAFUKWE WILAYA YA MAKETE MKOA WA NJOMBE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

UTANGULIZI.
Ninayofuraha kubwa sana kukujulisha kwamba umechaguliwa kidato cha kwanza katika shule ya sekondari MOUNT CHAFUKWE mwaka 2021. Shule ya Mount Chafukwe ipo katika kata ya Mfumbi, Wilaya ya Makete kando kando kabisa na barabara kuu ya Mbeya – Dar es salaam. Shule hii ni ya kutwa, ila inayo nafasi chache za hostel kwa wasichana tu.

Shule itafungua tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi (1:00) siku ya jumatatu, tarehe hiyo fika shuleni na mzazi/ mlezi wako ukiwa umekamilisha sare ya shule inayotakiwa kama utakavyoelekezwa hapo chini.

SARE ZA SHULE:

A) WAVULANA

- Suruali moja rangi ya KAKI na suruali ya pili rangi ya DAMU YA MZEEE, zote ziwe na marinda mawili kila upande, suruali zisiwe za kubana wala zisiwe fupi la sivyo hautapokelewa.
- Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mifupi. Shati moja iwekwe nembo ya damu ya mzee kwenye kora na shati lingine liwekwe nembo ya kaki kwenye kora.
- Kiatu cheusi chenye kisigino kifupi cha kufunga na kamba. Soksi ziwe rangi ya kijivu.
- Mkanda wa kuvalia suruali uwe wa rangi nyeusi tu.

B) WASICHANA

- Sketi mbili (rangi ya kaki na rangi ya damu ya mzee) ziwe ndefu zinazoweza kugusa kiatu (sketi fupi utarudishwa nayo nyumbani), zishonwe kwa mshono unaoitwa rinda box.

- Shati mbili (2) nyeupe zenye mikono mifupi. Shati moja iwekwe nembo ya damu ya mzee kwenye kora na shati jingine liwekwe nembo ya kaki kwenye kora.
- Kiatu cheusi cha ngozi chenye kisigino kifupi ambacho ni kiatu cha kufunga na kamba. Soksi ziwe rangi nyeupe tu.

C) KWA WOTE (WAVULANA NA WASICHANA)

- Sweta moja rangi ya zambarau
- Daftari counterbook Q2 ziwe 10 kwa kuanzia, rula ya plastic, pen, kalamu na kibweta cha hisabati (mkebe wenye vifaa ndani)
- Kupitia mapatano ya wazazi ili wanafunzi waweze kufanya mitihani mingi sana ya majaribio, kila mwanafunzi ataleta bunda moja la karatasi kwa mwaka (ream paper) size A4.

MICHANGO YA CHAKULA

Wilaya yetu na shule yetu pia inasisitiza kuwa mwanafunzi awapo shuleni apate chakula, jukumu la kutoa chakula ni la mzazi wa mwanafunzi husika hivyo kupitia vikao vya wazazi, michango ifuatayo ya chakula ilikubaliwa;

A) WANAFUNZI WATAKAOPATA NAFASI YA KUKAA HOSTEL.

Michango ya chakula kwa mwanafunzi atakayekaa hostel (WASICHANA TU) ni kama ifuatavyo;-(kwa mwaka)

- Pesa taslimu 96,000/= (elfu tisini na sita tu)
- Mahindi debe 5
- Maharage debe 2
- Mchele debe 2
- Mafuta ya kupikia lita 3
- Sukari kg 4
- Chumvi paketi 4

Mahitaji mengine kwa wasichana wa hostel;-

- Mashuka mawili (moja pink na jingine blue bahari kwa ajili ya kutandika kitandani.
- Chandarua cha duara, rangi nyeupe
- Mashuka mengine ya kujifunika
- Vitu kama mswaki, dawa ya meno, sabuni, kandambili na vifaa vya kuogea kwa ujumla.
- Ndoo mbili za kuhifadhia maji (ziwe za plastic za lita 10), tochi kwa matumizi binafsi.
- Kidumu cha kutunzia maji ya kunywa angalau cha lita 5,(matumizi binafsi).
- Gauni la rangi ya DARK BLUE mshono wa solo.(shamba dress)
- Tracksuit nyeusi yenye michirizi myeupe aina ya adidas.

NB: Mwanafunzi wa hostel haruhusiwi kuja na nguo nyingine za nyumbani.

B) WANAFUNZI WA KUTWA (DAY)
(WASICHANA NA WAAVULANA)

- Pesa taslimu Tshs. 25,000/= (elfu ishirini na tano tu)
- Mahindi debe 3
- Maharage debe 1
- Mafuta lita 2
- Sukari kg 4
- Chumvi packet 4

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KUHUSU MICHANGO YA CHAKULA

i) Michango ya chakula ni ya lazima kwa kila mzazi kumtolea mtoto wake.

ii) Mwanafunzi ataanza kula chakula shuleni pale mzazi atakapotoa michango angalau robo ya michango anayodaiwa kwa mwaka.

iii) Hakuna kupunguziwa michango hata kama mtoto au mwanafunzi atachelewa kuanza kula kwa uzembe wa mzazi kutokutoa michango kwa wakati.

iv) Pesa zote za chakula zipelekwe bank ya NMB au wakala wa NMB namba ya akaunti 60410000695-MOUNT CHAFUKWE SEKONDARI.
Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye stakabadhi ya malipo (BPS) kisha lete shuleni nakala ya malipo hayo.

Mwisho unahimizwa kumwandikisha mtoto wako kwenye mfuko wa afya CHF ili pindi mtoto akiugua apate matibabu kwa urahisi, hapa shuleni tunahuduma ya kwanza tu (hakuna matibabu).

"UNAKARIBISHWA SANA MOUNT CHAFUKWE SEKONDARI"

.....
SIMON A. MWAMBAGI
KAIMU MKUU WA SHULE
0752494822 / 0623549101

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

1. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;-
   a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
   b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
   c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
   d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
   e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
   f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
   g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
   h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
   i) Kutunza mali za umma.
2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.
   a) Wizi
   b) Uasheraati na ushoga
   c) Ubakaji
   d) Ulevi na matumizi yaa dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
   e) Kupigana au kupiga
   f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   g) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba
   h) Kuoa au kuolewa
   i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
   j) Kukataa adhabu kwa makusudi
   k) Kuwa/ kumiliki simu ya mkononi.
3. Mambo mengine yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na wanafunzi.
   a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
   b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
   c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

"KARIBU SANA KATIKA SHULE HII"

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi _____ nakiri kwamba nimesoma na kuyaelewa masharti na sheria za shule kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 kwamba kwa uwezo wangu wote nitafuata na kutekeleza kanuni na sheria za shule kipindi chote niwapo shuleni, hivyo nitakuwa mtiifu daima.

Dini yangu ni _____ Dhehebu _____

_____ _____ _____

Jina Saini Tarehe

AHADI YA MZAZI

Mimi _____ ambaye ni mzazi/ mlezi wa _____ nakubali/ sikubali nafasi aliyopewa mwanangu katika shule ya sekondari Mount chafukwe na ninaahidi kutimiza mahitaji yake yote na pia nitashirikiana na uongozi wa shule na serikali katika kulea na kumtunza mwanafunzi mpaka atakapomaliza masomo yake ya sekondari.

Dini yangu ni _____ Dhehebu _____

_____ _____ _____

Jina Saini Tarehe

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE – RALG
MAKETE DISTRICT COUNCIL

MOUNT CHAFUKWE SEC. SCHOOL,
P.O BOX 55
CHIMALA – MBEYA.
04/12/2020

REF.NO.MTCSS/JI/2021
THE MEDICAL OFFICER,
_____
_____
_____

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Kindly examine (Name) _____ to determine on her/his physical and mental fitness to pursue secondary studies at Mount Chafukwe Secondary.

_____
THE HEADMASTER

1. Eyesight _____
2. Hearing _____
3. Speech _____
4. Limb _____
5. Leprosy _____
6. Epilepsy _____
7. Cardiac disease _____
8. Rheumatism _____
9. Venereal _____
10. Pregnancy (for girls) _____
11. Any other serious disease _____
12. Any disabilities _____

General comments _____
_____

Name _____ signature _____

Designation _____ Stamp _____ Date _____

NB: Fomu hii inatakiwa mwanafunzi aende/ uende naye akapime kwa daktari wa zahanati/ kituo cha afya/ hospitali inayotambulika na serikali na kisha uilete shuleni unavyokuja na mwanao siku ya **tarehe 11/01/2021.**

SHULE YA SEKONDARI MOUNT CHAFUKWE
FOMU YA MAELEZO BINAFSI YAHUSUYO MWANAFUNZI

A) 1. Jina la mwanafunzi _____
   2. Tarehe ya kuzaliwa _____
   3. Mahali alipozaliwa (wilaya) _____ mkoa _____

B) 1. Baba mzazi yupo hai? _____ Ndiyo/ Hapana
   2. Mama mzazi yupo hai? _____ Ndiyo/ Hapana

C) 1. Jina la mzazi/ mlezi anayekulea _____
   2. Kazi ya mzazi/ mlezi _____
   3. Anuani ya mzazi/ mlezi _____
   4. Namba za simu ya mkononi _____
   5. Mahali ambapo anaishi mzazi/ mlezi _____

Kijiji _____ mji _____

Wilaya _____ mkoa _____

D) Majina na anuani za ndugu wengine wa karibu wanaohusika na malezi ya mwanafunzi.
   1. Ndugu _____ uhusiano _____ simu_____
      Anuani _____

   2. Ndugu _____ uhusiano _____ simu_____
      Anuani _____

   3. Ndugu _____ uhusiano _____ simu_____
      Anuani _____

E) Anuani ya kiongozi yeyote wa kata/ kijiji/ mtaa ambako mzazi wa mwanafunzi anaishi.
   Cheo cha kiongozi _____
   Kata ya _____
   Anuani yake _____ namba ya simu _____
   Jina _____ saini _____